ACT WAZALENDO

# TANZANIA TUNAYOIPIGANIA

## CHAMA CHA WAZALENDO



2015

# 1. UTANGULIZI: ITIKADI, FALSAFA NA IMANI YA ACT

1.1 ACT inaamini katika misingi ya Ujamaa wa kiDemokrasia (Democratic Socialism) ikiwa na ngao tatu zifuatazo:

1) Undugu ni hifadhi ya jamii ya asili kwa Afrika, na hivyo kila mtanzania na kila mwafrika ana jukumu la kumsaidia mwenzake anayekabiliwa na tatizo au janga popote alipo bila kutarajia malipo ya aina yoyote;

2) Serikali ina haki na wajibu wa kutengeneza sheria na kanuni zenye kulenga kuleta usawa wa kibinadamu katika jamii. Aidha, Serikali ina haki na wajibu wa kusimamia moja kwa moja sekta nyeti katika jamii zenye maslahi mapana ya kiusalama na kiuchumi kwa nchi; na

3) Viongozi na watumishi wa umma wana wajibu wa kuhakikisha kwamba wanaishi na kuenenda katika misingi inayolinda heshima ya ofisi za umma na kwamba hawatumii nafasi zao kwa manufaa yao binafsi na jamaa zao. Ili kuwasaidia na kuwawezesha viongozi na watumishi wa umma kuenenda katika misingi ya uadilifu, kuna haja ya kuwekewa miiko na maadili maalum ya viongozi.

1.2 ACT inatambua kuwa sisi wananchi wa Tanzania ndiyo raslimali kubwa ya nchi, na kwamba nchi yetu imejaliwa raslimali nyingi ambazo zikivunwa na kutumika vizuri zinaweza kuboresha maisha na kuchangia katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, shabaha kuu ya ACT ni kuhakikisha kuwa utajiri wa nchi unatumika kuboresha maisha ya watu na kuchochea uwezo wao katika kuchangia kujenga uchumi shirikishi ambapo kila mtu ana fursa sawa za maendeleo.





1.3 Falsafa ya ACT ni UNYERERE, ikiwa ni dhamira ya kurudisha, kuhuisha na kupigania misingi mama iliyoasisi Taifa la Tanzania, kama ilivyoainishwa katika Azimio la Arusha na kwa mazingira ya Tanzania ya sasa, ikiwa na imani kwamba:

1) Binadamu wote ni sawa;

2) Kila mtu anastahili heshima;

3) Kila raia ana uhuru kamili wa kutoa mawazo yake, kwenda anakotaka na kuamini dini anayotaka na kukutana na watu wengine bila kuvunja sheria;

4) Kila mtu ana haki ya kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake na mali yake aliyo nayo kwa mujibu wa sheria;

5) Kila mtu anayo haki ya kupata malipo ya haki kutokana na kazi yake;

6) Raia wote kwa pamoja wanamiliki utajiri wa asili wa nchi hii ukiwa kama dhamana kwa vizazi vyao na vizazi vijavyo; na

7) Serikali ina mamlaka na wajibu wa kusimamia njia muhimu za kukuza uchumi.

## 2. MISINGI YA ACT

ACT inaongozwa na Misingi Kumi (10) ifuatayo:

### 1. Uzalendo

Sisi wananchi wa Tanzania tunaipenda nchi yetu. Uzalendo ndio moyo wa kuanzishwa kwa ACT. Zaidi ya kuipenda nchi yetu, uzalendo ni juu ya kile ambacho tunadhamiria kukifanya na kujitoa katika kuitumikia na kuilinda nchi yetu. Hivyo basi, ubora na umakini wa maamuzi yetu kama chama utapimwa kwa kuangalia ni namna gani maamuzi hayo yana faida kwa taifa letu na wananchi wake leo na kesho.



### 2. Utu

Sambamba na Katiba ya Nchi yetu na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu ambalo nchi yetu imelikubali, utu ni msingi mama kwa ACT. Tunatambua thamani ya asili ya ubinadamu na haki za msingi na za asili ambazo binadamu wamepewa tangu uumbaji. Tunaamini kwamba utu ndio msingi wa uhuru, haki, amani na ustawi wa jamii. Tumedhamiria kupigania, kulinda na kuendeleza maendeleo ya jamii na ustawi wa watu wote na tutapigania na kuheshimu haki za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni kwa watu wote.

### 3. Kupinga ubaguzi

Ubaguzi ni adui wa utu na tutaupinga kwa nguvu zote wakati wote na mahala popote. Tunaamini kwamba kila binadamu anastahili heshima na hastahili kubaguliwa kwa sababu ya kabila, rangi, jinsi, lugha, dini, chama cha siasa, utaifa, hali ya kiuchumi, familia anayotoka, afya, ulemavu, n.k.. Tunaamini kwamba kila mtu anastahili kupata haki na kwamba maslahi ya makundi yote lazima yazingatiwe katika utungaji wa sera na sheria. Kutokuwa na ubaguzi ni msingi muhimu katika kujenga utaifa na maendeleo shirikishi.

### 4.Usawa

Kutokana na miaka mingi ya ubaguzi wa kiuchumi na kijinsia, nchi yetu kwa sasa inapita katika wakati ambao kuna pengo kubwa la kipato kimaisha na kijamii kati ya maskini, ambao ni kundi kubwa, na matajiri wakiwakilishwa na kundi dogo. Bila kuchukua hatua stahiki sasa maskini watazidi kuwa maskini. ACT imeundwa katika misingi na imani kwamba kila mtu anafurahia matunda ya bidii yake katika kazi, na kwamba bidii na umakini katika kazi ndiyo chanzo cha mafanikio kwa kila raia. Tunaamini kwamba tunahitaji kuhuisha misingi ya usawa kwa kuweka mazingira sawa na kuwekeza katika kundi la watu ambao wameachwa nyuma na kunyimwa fursa za kujiendeleza.





Tunaamini ni jukumu na wajibu wa serikali kuhakikisha usawa katika jamii kwa kuchukua hatua stahiki za kuwainua wale ambao wapo nje ya mstari na hawafaidiki na ukuaji wa uchumi wa taifa.

### 5. Demokrasia

Msingi mama wa demokrasia ni kuhakikisha kuwa sauti za watu zinasikika na kuzingatiwa katika mipango ya maendeleo ya nchi. Tunaamini kwamba ni wananchi pekee wenye uhalali wa kuamua nani awaongoze na aina ya viongozi wanaowataka. Kama chama, kwetu dhana ya demokrasia inakwenda zaidi ya chaguzi za mara kwa mara. Dhana ya demokrasia kwa ACT ni sehemu ya mfumo wa uendeshaji wa chama ambapo kila mwanachama anayo nafasi na fursa ya kuchangia katika maamuzi ya chama na nchi, na anayo haki ya kuomba kuchaguliwa katika ngazi yoyote ya uchaguzi.

### 6. Uhuru wa Mawazo na Matendo

Jamii yoyote ya kidemokrasia inategemea uwepo wa uhuru wa kutofautiana kimawazo na fursa ya kila mtu kutoa maoni yake bila woga. Tunaamini kwamba watu wanapaswa kuwa na uhuru wa matendo ili mradi tu matendo yao hayaingilii haki za watu wengine wala kuvunja sheria. Tunaamini kwamba ubunifu ni zao la mchango wa mawazo tofauti kutoka kwa watu tofauti. Hivyo, chama kitalea na kuhamasisha utamaduni wa uhuru wa mawazo kama njia ya kuendelea kujifunza njia bora zaidi za kuboresha maisha ya watanzania.

### 7. Uadilifu

Tunaamini kwamba kura ni tendo la imani linaloonyeshwa na mwananchi kwa viongozi anaowachagua. Uaminifu wa wananchi unapaswa kuheshimiwa kwa kuonyesha uadilifu wa hali ya juu kutoka kwa viongozi.



Sisi kama chama tutasimamia uadilifu kwa umakini mkubwa kama njia muhimu ya kujenga imani na kuwapa heshima wale wanaotuamini katika kuwatumikia. Ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza msingi huu kikamilifu, tumetengeneza kanuni za mwenendo wa maadili na miiko ya uongozi ambayo kila kiongozi wa ACT atasaini kukubaliana kuwajibishwa kwayo. Maadili na miiko ya uongozi itakuwa ndiyo dira ya mwenendo wa viongozi wote wa ACT katika utumishi wa umma na ambao tungependa umma wa watanzania utuwajibishe nao.


### 8. Uwazi

Ili wananchi waweze kuwawajibisha viongozi wao ni lazima wawe na taarifa sahihi na kwa wakati unaofaa. Tunaamini kwamba wananchi wana haki ya kupata taarifa sahihi na kwa wakati kutoka kwa viongozi wao na ofisi zote za umma kwa kuwa viongozi wanafanya kazi na kusimamia raslimali za chama na taifa kwa niaba ya wananchi. Katika kutekeleza msingi huu, viongozi wote wa ACT watapaswa kueleza mali wanazomiliki kwa wanachama na wananchi katika maeneo yao ya uongozi, kabla na baada ya kuchaguliwa au kuteuliwa. Aidha, programu zote za chama pamoja na mapato na matumizi zitawekwa wazi kwa umma na wanachama na wananchi wataruhusiwa kuzikagua wakati wowote.

### 9. Uwajibikaji

Bila kujenga utamaduni wa kuwajibishana hatutaweza kama taifa kujenga jamii ambayo kila mtu anaheshimiwa na kuheshimu sheria ambazo tumejiwekea. Uwajibikaji unapaswa kuanza na viongozi waliopewa dhamana ya kuongoza harakati za mabadiliko katika nchi. Katika ACT, tunaamini kwamba kila mtu anayetupigia kura ametuamini na kuweka matumaini yake kwetu kwamba tunaweza kutekeleza kile tunachosema.





Tunaamini pia kwamba wanachama na viongozi wanapaswa kuwajibishwa kwa matendo na ahadi wanazozitoa kwa wananchi.

**10. Umoja**

Umoja ndiyo nyenzo muhimu ya kukabiliana na changamoto ambazo zinatukabili leo na kesho. Kama nchi ambayo imejaliwa utajiri na tofauti za kijamii mbalimbali kama vile utamaduni, kabila, dini, lugha, na siasa, tunahitaji kusimama pamoja ili kuweza kujenga taifa moja la Tanzania ambalo kila mmoja anafurahia kuwa sehemu yake. Kwa hiyo mapambano na shida za kundi moja ni mapambano na shida zetu sote. Kwa kuzingatia historia yetu ya kupigania umoja na maelewano katika bara la Afrika na duniani kwa ujumla, ACT inatambua umuhimu wa umoja na ushirikiano na majirani zetu na hivyo itashirikiana na nchi nyingine katika kusukuma mbele ajenda ya Umoja wa Afrika ili kuweza kujenga nguvu za pamoja katika kujiendeleza kiuchumi, kiuta-maduni na kisiasa.

Copyright Freddy Feruzi





# 3. TANZANIA TUNAYOIPIGANIA

3.1 Tanzania ni zaidi ya mkusanyiko wa watu na vitu vilivyomo. Msingi wa ujenzi wa Taifa ulikuwa ni UZALENDO uliochochewa na itikadi, falsafa na imani imara.

3.2 Hata hivyo, katika siku za karibuni utaifa wa Taifa la Tanzania umetikiswa. Nchi sasa imeanza kugeuka kuwa mkusanyiko tu wa watu wanaohangaika kutafuta vitu na ambao wanatumia muda mwingi kuimarisha 'vitaifa' vyao kupitia vyama vyao vya siasa, dini zao na hata kabila zao.

3.3 Kuna haja ya kufufua uzalendo, upendo, umoja na mshikamano wa watanzania wote bila kujali rangi, kabila, dini, jinsia na wala ufuasi wa chama cha siasa.

3.4 ACT tunataka kufufua utaifa wa Tanzania ili kila Mtanzania aone kuwa ana wajibu wa kujenga nchi yake kwa ajili ya leo na vizazi vijavyo.

3.5 Serikali itakayoundwa na ACT itaweka vipaumbele vitakavyochochea uwajibikaji na tija ya haraka kwa kila mtanzania, na kuhakikisha kwamba uchumi unaendelea kukua kwa kasi na kiwango ambacho kila mtanzania anaona matunda ya kukua kwa uchumi huo.

# 4. HAIBA NA TASWIRA YA SERIKALI YA ACT

Haiba na taswira ya serikali ya ACT itaonekana katika maeneo manne yafuatayo:

**1) Serikali inayowajibika na kuwaheshimu wananchi kupitia matokeo ya kazi zake:** Katika kutekeleza hili:

a. Kila wizara itakuwa na mpango kazi wenye malengo mahsusi na utakaowekwa wazi kwa umma. Utendaji na ufanisi wa kila wizara utapimwa kwa kuzingatia mpango huo wa kazi

b. Bajeti ya serikali na wizara zote itapangwa kwa kuzingatia mpango kazi wenye malengo mahsusi na viashiria vya matokeo vinavyopimika

**2) Serikali inayoheshimika kwa kuundwa na viongozi wazalendo, weledi na wachapa kazi.** Viongozi ambao hawana mawaa katika jamii na ambao watarudisha heshima ya Tanzania katika ramani ya ulimwengu na kufanya wananchi waipende na kuitumikia nchi yao kwa moyo na bidii

**3) Serikali inayochukizwa na kupambana na wala rushwa kwa vitendo.** Ili kutekeleza hili tutahakikisha kwamba:

a. Kila mtu anatii na kuzingatia utawala wa sheria

b. Watumishi wa umma wanaajiriwa kwa mujibu wa sifa za weledi na bidii katika kazi na wanapata mafunzo stahiki kwa ajili ya kuimarisha utendaji wao

c. Hatua za kisheria na kinidhamu zinachukuliwa haraka kwa wale wote wanaopatikana na vitendo vya kula rushwa

d. Kila kiongozi wa umma na wa chama atafuata kanuni maalum za maadili kwa kuweka wazi maslahi yao kupitia tangazo la mali na madeni ambalo litawekwa wazi kwa wananchi wote kuona, kuhoji na mfumo wa malalamiko juu ya usahihi wa tamko.

**4) Serikali ya uwazi na inayowajibika kwa wananchi.** Serikali itahakikisha kwamba kila uamuzi unaochukuliwa na serikali unajulikana kwa wananchi. Utii wa serikali ya ACT utakuwa kwa wananchi. Kila uamuzi utakaochukuliwa utapimwa kwa kigezo cha 'Uamuzi huu una maslahi gani kwa wananchi na nchi, sasa na baadaye'.



# 5. VIPAUMBELE VYA SERIKALI YA ACT

Serikali ya ACT itawajibika kwa wananchi na Taifa kwa kuwekeza katika maeneo manne ya kipaumbele yafuatayo:
1) Hifadhi ya jamii
2) Uchumi shirikishi wenye kuzalisha Ajira nyingi na bora
3) Afya
4) Elimu

## 5.1 Hifadhi ya Jamii

Hifadhi ya jamii ni mfumo imara na endelevu wa kuwajengea uwezo na utayari wananchi katika kukabiliana na matatizo na majanga ya kiuchumi na kijamii. Hifadhi ya jamii husaidia sana kutoa usalama na uhakika wa kiuchumi, kijamii na kiafya. Hii ni njia ambayo serikali, mwajiri na mwajiriwa huchangia kiasi fulani cha mapato yake ya sasa kwa ajili ya kumsaidia baadaye atakapokuwa hana uwezo wa kupata kipato cha uhakika. Aidha, hifadhi ya jamii husaidia wafanyakazi katika sekta ya umma na binafsi kukabiliana na gharama za matibabu na matatizo mengine ya kijamii. Tafiti zinaonyesha kuwa uwepo wa hifadhi ya jamii kwa watu wengi iwezekanavyo katika nchi huchangia kupunguza hali ya umaskini na hivyo kuipandisha nchi kiuchumi na kijamii. Hifadhi ya Jamii pia huchochea uwekaji akiba katika nchi na hivyo kuwezesha uwekezaji wa ndani na kupanua shughuli za uzalishaji mali.

Hapa Tanzania hifadhi ya jamii hupatikana kwa wananchi walioajiriwa pekee katika sekta ya umma na binafsi. Kwa sababu hii ni asilimia 6 tu ya nguvu kazi ya Watanzania ndiyo waliopo katika mfumo rasmi wa hifadhi ya jamii. Ndiyo kusema, watu wengi nchini hawana namna rasmi ya kujiandaa na namna ya kuishi baada ya kuishiwa nguvu za kufanya kazi kwa sababu ya uzee, magonjwa au ulemavu. Hii inachochea umaskini kwa sababu kundi kubwa la watu wanaostaafu hujikuta hawana namna ya kuishi na hivyo kutumbukia katika wimbi la umaskini. Aidha, kukosekana kwa mfumo rasmi wa hifadhi ya jamii kumefanya watu wengi wasiwe na uwezo na mfumo mzuri wa matibabu.

Ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kuingia katika mfumo wa hifadhi ya jamii, Serikali ya ACT itachukua hatua zifuatazo:

1) Kuanzisha mfumo ambao kila Mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 60 na kuendelea kupata pensheni.

2) Kupanua hifadhi ya jamii na kufikia wakulima, wafugaji na wananchi wengine waliojiajiri kwa kutunga sheria itakayopelekea Serikali kuchangia theluthi moja ya kila mchango wa mwananchi atakayechangia kima cha chini cha michango kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

3) Kutunga Sheria kuwezesha mifuko ya hifadhi ya jamii kutoa mafao ya bima za mazao na majanga kwa kilimo na mifugo na pia mfumo wa bei (price stabilization).

4) Kuboresha sheria za hifadhi ya jamii kwa kuhakikisha kuwa kila mwanachama anayechangia anapata bima ya afya kupitia Mfuko wa Bima wa Afya utakaoboreshwa pia.

5) Kuweka mfumo thabiti wa kuhakikisha wajibu wa Serikali katika kuhudumia watoto yatima na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu.

6) Kuhamasisha wananchi wajielimishe kuhusu umuhimu na namna ya kushiriki katika hifadhi ya jamii

**5.2. Uchumi shirikishi wenye kuzalisha Ajira nyingi na bora**

Watanzania walio wengi bado wanategemea kilimo cha asili kama ajira yao. Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), sekta ya kilimo cha asili inaajiri takribani robo tatu (75%) ya watanzania wote. Kwa vijijini asilimia 89 ya wananchi wanategemea kilimo wakati mijini ni asilimia 44. Kwa upande wa miji mikubwa kama vile Dar es Salaam asilimia kubwa (38%) ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi wamejiajiri wenyewe au wapo katika ajira zisizohusiana na kilimo. Fursa za ajira katika mfumo rasmi bado ni finyu sana.

Tafiti zinaonyesha kuwa tatizo la ajira nchini Tanzania na nchi zingine za kiAfrika ni ukosefu wa maarifa na stadi za kazi zinazowafanya wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu wasiajirike. Aidha, ufinyu wa sekta za uzalishaji na huduma unasababisha ufinyu wa nafasi za ajira. Ifikapo mwaka 2030 kutakuwa na watu milioni 25 zaidi katika soko la ajira, wastani wa watu milioni 1.6 kuingia katika nguvu kazi ya Taifa kila mwaka. Iwapo Taifa halitakuwa na mipango sahihi, badala ya kufaidika (demographic dividend), tutapata janga kubwa na machafuko.



Copyright Freddy Feruzi



Ili kukabiliana na ukosefu wa ajira nchini, Serikali ya ACT inalenga kutengeneza Taifa linalofanya kazi (a working nation) kwa kuchukua hatua zifuatazo:

1) Kuchochea uzalishaji viwandani kupitia:

a. Kuchochea uwekezaji katika viwanda vyenye kutoa ajira nyingi (light manufacturing industries) na viwanda vya msingi vinavyotumia maliasili tuliyonayo hapa nchini;

b. Kuchochea uchumi wa vijijini kwa kujikita katika kuongeza thamani ya mazao ikiwemo kusindika mazao ya mashambani na mifugo. Serikali itatoa nafuu ya kikodi (tax credits) kwa wanaouza nje bidhaa za kilimo zilizosindikwa nchini;

c. Kuweka utaratibu wa kisheria wa kutoa ruzuku ya gharama za umeme kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa za matumizi muhimu ya wananchi kama Sukari ili kuvifanya vishindane na tishio la bidhaa hizo kutoka nje ya nchi na kulinda ajira za Watanzania;

d. Kupiga marufuku kuuza nje bidhaa ghafi za Pamba, Korosho, Mkonge na ngozi. Kabla ya marufuku hiyo Serikali itaweka kipindi cha mpito cha miaka 3 cha uwekezaji na ufufuaji wa viwanda katika sekta ndogo hizo.

2) Kuwa na utaratibu maalumu wa kisheria utakaohakikisha kwamba bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini zinatumiwa na serikali na taasisi zake. Ofisi za serikali hazitaruhusiwa kutumia samani na bidhaa za nje kama bidhaa hizo zinaweza kuzalishwa hapa nchini

3) Tutaweka sera inayohakikisha kwamba angalau asilimia 20 ya manunuzi yote ya serikali na taasisi zake zinatokana na miradi ya kiuchumi na kibiashara inayoendeshwa na vijana

4) Kuhakikisha kwamba kuna uwiano mzuri kati ya mfumo wa elimu rasmi na elimu ya ufundi ili kuhakikisha kwamba vijana wanaomaliza katika taasisi za elimu wanakuwa na maarifa na stadi za kazi

5) Kuhakikisha kwamba mfumo wa manunuzi (tenda) wa serikali unakuwa wazi na bila rushwa ili kuhakikisha kwamba vikundi vya kijasiriamali vya vijana na akina mama vinaweza kupata tenda zinazotolewa na serikali katika maeneo mbalimbali

6) Serikali itatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli za maendeleo ili kuchochea shughuli za uzalishaji na ujenzi wa miundo mbinu ambazo zinatoa nafasi za ajira. Ili kufikia lengo hili, serikali itabana matumizi ya kawaida kwa kuondoa matumizi yasiyo ya lazima kama vile posho za vikao na kuachana na matumizi ya magari ya kifahari kwa maafisa na viongozi wa serikali na taasisi zake.

7) Kuhamasisha na kutoa msukumo wa kikodi kuanzishwa kwa taasisi ndogo ndogo za fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa ajili ya biashara mpya na shughuli zingine za ujasiriamali miongoni mwa vijana na akina mama

8) Kwa kuwa serikali ndiye mwajiri mkubwa, tutaweka utaratibu wa mafunzo kazini (internship) kwa wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu kupewa fursa ya kuhudhuria katika taasisi mbalimbali za umma kwa lengo la kujifunza kazi wakati wakiendelea kutafuta fursa za ajira.



## 5.3 Afya

Tanzania ni nchi kubwa na yenye idadi kubwa zaidi ya watu katika ukanda wa Afrika Mashariki. Pamoja na kwamba uchumi umekuwa ukikua kwa takribani asilimia saba (7) kwa mwaka, ukuaji huu haujionyeshi katika kuboreka kwa hali ya maisha ya wananchi wa kawaida. Kwa mujibu wa Taarifa ya Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, kumekuwa na ongezeko la idadi ya watu kufikia asilimia 3 kwa mwaka na idadi ya watu ambao wanaishi katika umaskini wa kutupwa (ufukara) imeongezeka kwa idadi ya zaidi ya watu milioni moja. Ongezeko hili la idadi ya watu maskini linamaanisha ongezeko la watu ambao wanashambulika zaidi na magonjwa yanayozuilika na ambao watahitaji zaidi huduma za afya sasa na katika siku za usoni. Hata hivyo kiasi kidogo cha fedha kimekuwa kikitengwa kwa ajili ya huduma za afya.

Idadi ya vifo vya watoto wachanga na mama waja wazito bado ipo juu na tumeshindwa kufikia malengo ya Millenia. Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya za mwaka 2013, takribani akina mama 450 kati ya 100,000 wanaojifungua hufa na asilimia 43 tu ya akina mama waja wazito hupokea huduma za Kliniki ya waja wazito, na asilimia 51 pekee ya mama waja wazito hujifungua kwa msaada wa wataalamu wa afya.

Idadi kubwa ya watanzania bado wapo katika hatari ya kuambukizwa au kupata magonjwa yanayozuilika kama vile malaria na UKIMWI. Malaria ndiyo ugonjwa unaoua watanzania wengi zaidi (hasa watoto wachanga) ukifuatiwa na UKIMWI na kifua kikuu, na yote haya ni magonjwa yanayozuilika na kutibika na/au kudhibitika. Kwa mfano, inakadiriwa kuwa watanzania milioni 1.6 wanaishi na VVU/UKIMWI na kila mwaka zaidi ya watu 100,000 huambukizwa na zaidi ya watu takribani 86,000 hufa kila mwaka kutokana na UKIMWI. Hii imesababisha watoto zaidi ya milioni 1.5 kuwa yatima na kuhitaji hifadhi ya kijamii. Tanzania ni nchi ya 15 kati ya nchi 22 zenye wagonjwa wengi wa kifua kikuu (TB) na hii ndiyo sababu kubwa ya vifo kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI.



Idadi ya wananchi wanaougua magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile magonjwa ya moyo, figo, kisukari na kansa imeongezeka. Magonjwa haya yanaweza kuepukika kwa kuwa na mfumo wa ugunduzi wa mapema katika ngazi ya msingi.

Tanzania pia ni miongoni mwa nchi katika bara la Afrika zenye idadi ndogo zaidi ya wataalamu wa afya. Kwa mfano, kwa takwimu za mwaka 2010 kuna madaktari 0.4 na wauguzi/wakunga 2.8 kwa kila watu 10,000, ukilinganisha na wastani wa madaktari 2.8 na wahudumu 6.7 kwa nchi zinazoendelea.Ukosefu wa wataalamu wabobezi na vifaa tiba umesababisha wananchi kupelekwa nje kwa ajili ya matibabu na hivyo kugharamiwa kwa fedha nyingi.

Sekta ya afya pia inakabiliwa na kuchakaa kwa miundo mbinu na ukosefu wa huduma za msingi kama vile madawa, vifaa tiba, vitendanishi na vitanda katika wodi za wagonjwa. Kutokana na uchakavu wa miundo mbinu na kukosekana kwa huduma za afya katika mahospitali ya umma, wananchi wengi hawaoni kama hospitali ni sehemu salama ya kupata huduma. Matatizo haya kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na ukosefu wa raslimali fedha, vitendo vya rushwa na kukosekana kwa ubunifu na uongozi bora katika hospitali za umma.

Takwimu za mashirika ya kimataifa za mwaka 2013 zinaonyesha kuwa ni nusu tu ya watanzania wote ndio wanaopata maji safi na salama, na hali ni mbaya zaidi kwa upande wa vijijini. Watoto 10,000 hufa kila mwaka kutokana na kipindupindu kwa kunywa maji yasiyo salama. Hali hii humuongezea mama ugumu wa maisha kwa kuwa anatumia muda mwingi kutoa huduma nyumbani badala ya kufanya kazi za uzalishaji.

### 5.3.1 Mpango wa ACT kuhusu Afya

Katika kukabiliana na changamoto za afya zilizoainishwa hapo juu na kuboresha huduma za afya, falsafa itakayoongoza sekta ya afya chini ya Serikali ya ACT ni kuwekeza katika huduma za kinga. Serikali itachukua hatua zifuatazo katika kuimarisha sekta ya afya:

1) Kuchukua hatua za dharura katika kuimarisha huduma za mama na mtoto katika vituo vya afya ili kuzuia vifo vya watoto na mama wajawazito, ikiwemo:

a. Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wahudumu wa afya katika vituo vya afya na hospitali zote

b. Huduma zote za msingi kuhusu afya ya watoto na mama wajawazito zitakuwa bure katika hospitali za umma na binafsi. Katika siku 100 za mwanzo za utawala wa ACT, itaundwa Tume ya Wataalamu katika sekta ya afya na uchumi kuainisha huduma za msingi za afya kwa mama na mtoto ambazo serikali ikizigharamia zitaleta tija katika kumaliza vifo visivyo vya lazima kwa watoto na mama wajawazito.

2) Kufufua na kuimarisha mfumo wa huduma za afya ya msingi ikiwemo elimu ya afya kwa jamii ya kitanzania na kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa usawa na kwa wakati.

3) Kujikita kwenye afya ya kinga kwa jamii kwa kutumia mbinu shirikishi na kuibua mipango yenye tija.

4) Kupitia upya sheria iliyoanzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kumwezesha na kuhakikisha kuwa kila mwananchi anakuwa na haki ya matibabu na huduma za afya kupitia mfumo wa umma

5) Serikali itatenga bajeti maalumu kwa ajili ya kupanua mafunzo ya kada zote za afya katika vyuo vikuu vya umma na kuweka ushirikiano maalum na vyuo vya binafsi vya afya ili viweze kutoa wataalamu wengi zaidi katika fani za afya. Serikali itaanzisha 'scholarship' maalum ya kupeleka watumishi wa afya kwenda kusomea utabibu katika vyuo vya nje kwa maeneo ambayo utaalam huo haupatikani hapa nchini.

6) Kupitia upya muundo wa mishahara ya watumishi katika sekta ya afya ili kutoa motisha zaidi kujiunga na kubaki katika sekta hii

7) Kupitia na kuimarisha mfumo wa utengenezaji, uagizaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba ili kuhakikisha vinapatikanakwa ubora wa hali ya juu na kwa wakati. Viwanda vya ndani vya madawa vitapata nafuu maalum ya kikodi.

8) Bajeti ya Wizara ya Afya itakuwa 'ring fenced', ikishapitishwa na Bunge hapatakuwa na mamlaka nyingine yoyote ile itakayoipunguza.

9) Serikali itaimarisha ushirikiano na sekta binafsi ya afya ili kuongeza huduma za matibabu ambazo awali hazikuwepo nchini.

10) Kuanzisha mpango maalum wa miaka mitano wa kukarabati miundo mbinu ya hospitali za umma katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa kwa kuwashirikisha wadau wa maendeleo ndani na nje ya nchi

11) Kuanzisha mfuko wa maji vijijini (Rural Water Fund) utakaotumika kuendeleza na kulinda vyanzo vya maji vijijini na kukarabati miundo mbinu ya maji mijini na katika majiji

12) Wananchi watahamasishwa ili waendelee kujielimisha kuhusu umuhimu na namna ya kutunza vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla.





## 5.4 Elimu

### 5.4.1 Mtazamo wa ACT


ACT inaamini kwamba elimu ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo. Bila kuwekeza kikamifu katika elimu na kuhakikisha kwamba watu wengi iwezekanavyo wanapata fursa za elimu bora, mipango ya maendeleo haiwezi kufanikiwa. Tafiti nyingi zinaonyesha kwamba ili Taifa liweze kupiga hatua ya maana ya kimaendeleo ni muhimu elimu ya lazima iwe kwa wote kwa kipindi kisichopungua miaka kumi (elimu ya msingi na sekondari) na angalau asilimia isiyopungua 20 wawe na kiwango cha elimu ya juu.

Kiwango chetu cha elimu kwa maana ya idadi na ubora bado kinakabiliwa na changamoto nyingi ambazo bila kuzitatua mapema iwezekanavyo mchango wa sekta ya elimu katika maendeleo ya nchi hautaonekana, na kwa kweli hatutaweza kupiga hatua zozote za maana za kimaendeleo. Baadhi ya changamoto na matatizo katika sekta ya elimu ambayo Serikali ya ACT itayashughulikia kwa haraka ni hizi zifuatazo:

b) Kushuka kwa idadi ya watoto wanaojiuga na elimu ya msingi. Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa ni asilimia 78 tu ya watoto wenye umri wa kwenda shule ndiyo walioandikishwa katika shule za msingi. Hii ndiyo kusema zaidi ya asilimia 20 ya watoto wenye umri wa elimu ya msingi hawapo mashuleni

c) Zaidi ya asilimia 20 ya watu wazima wenye umri kuanzia miaka 15 hawajawahi kupata elimu yoyote rasmi nchini

d) Asilimia zaidi ya 50 ya watoto wanaomaliza elimu ya msingi hawapati fursa za kujiunga na elimu ya sekondari au ufundi



e) Ni asilimia 2.4 tu ya watanzania ndiyo wenye elimu ya juu kwa ngazi ya shahada ya kwanza. Idadi hii ni ndogo mno na inaifanya nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi tatu Afrika na duniani zenye kiwango kidogo cha watu wenye elimu ya juu

f) Uduni wa ubora wa elimu inayotolewa katika ngazi mbalimbali na hasa katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari. Tafiti zinaonyesha kwamba ni watoto watatu tu kati ya watoto kumi waliopo darasa la tatu ndiyo wenye uwezo wa kufanya mahesabu ya ngazi ya Darasa la Pili. Aidha, takribani watoto watatu kati ya kumi (30%) waliomaliza darasa la saba hana maarifa ya kumudu mahesabu ya darasa la pili. Katika miaka ya hivi karibuni ufaulu katika mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne yameshuka sana hadi pale serikali ya CCM ilipoamua kushusha kiwango cha ufaulu ili kuwawezesha wanafunzi wanaofeli kuonekana wamefaulu!

g) Unyonge wa watanzania kumudu lugha ya Kiingereza. Katika ukanda wa Afrika, ni watanzania pekee ambao hawamudu lugha ya Kiingereza na/au lugha nyingine ya kimataifa. Inakadiriwa kwamba ni asilimia 16 pekee ya watanzania ndiyo wanaoweza kuwasiliana kwa lugha zote mbili yaani Kiswahili na Kiingereza. Hali hii imekuwa ikikwamisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwa walimu na wanafunzi hawamudu somo la Kiingereza ambalo ndilo linalotumika katika elimu kuanzia elimu ya sekondari hadi elimu ya juu.

h) Kushuka kwa ari ya kujisomea miongoni mwa vijana wa Kitanzania, kutokana na, pamoja na sababu zingine, kutokuwepo vyanzo vya maarifa katika sehemu mbalimbali nchini na hasa vijijini



Copyright Freddy Feruzi



### 5.4.2 Mpango wa ACT

Ili kupanua fursa na kuboresha viwango vya elimu katika ngazi mbalimbali, Serikali ya ACT itachukua hatua zifuatazo:

1) Kuwahimiza wazazi na walezi katika kuhakikisha kwamba wanawapeleka watoto wao kuandikishwa shule, na kuweka utaratibu imara zaidi wa kisheria utakaotoa adhabu kwa wazazi/walezi ambao hawawapeleki watoto wao kuandikishwa shule

2) Kufufua mpango wa maktaba za jamii (community libraries) katika kila Jimbo

3) Ili kupanua wigo wa elimu ya lazima kufikia miaka 9-10 kama ilivyo kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya ACT itaanza utekelezaji wa sera mpya ya elimu inayounganisha mfumo wa elimu ya msingi na sekondari ili kufanya elimu ya msingi kuwa miaka 10

4) Kwa kuzingatia matokeo ya tafiti yanayoonyesha kuwa walimu ndio kisababisha kikubwa cha mafanikio ya elimu na katika kuwawezesha wanafunzi kujifunza, na kwamba motisha ni muhimu katika kuwachochea walimu kufanya kazi kwa bidii na weledi, Serikali ya ACT itaweka utaratibu maalum wa kimaslahi utakaovutia na kuwabakisha walimu katika kazi ya ualimu. Aidha, Serikali ya ACT itaweka mfumo wa motisha kwa walimu utakaozingatia utendaji na mafanikio katika kuwawezesha wanafunzi kujifunza (performance based incentive system). Aidha, serikali itaweka utaratibu mpya wa usimamizi kwa walimu ili kuhakikisha kwamba wanatekeleza wajibu wao kikamilifu.

5)Ili kupanua wigo wa elimu ya juu mapema iwezekanavyo, Serikali ya ACT itachukua hatua zifuatazo:

a. Kuanzisha mpango wa muda mrefu wa ujenzi wa vyuo vikuu katika kila kanda

b. Kuanzisha mfumo nyumbulisho wa usajili katika vyuo vikuu ili kuongeza idadi ya wahitimu wenye sifa za kujiunga na vyuo vikuu

c. Kuongeza idadi ya shule za sekondari ya juu (Advanced secondary schools) ili kupanua wigo wa wanafunzi wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu

d. Kuanzisha utaratibu wa kutoa scholarship katika vyuo vikuu vya umma kwa wahitimu wote wenye sifa za kujiunga na vyuo hivyo

6) Kufufua na kuimarisha mfumo wa mafunzo ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wote wanaojiunga na Kidato cha Kwanza

7) Katika kutafuta suluhu ya muda mrefu katika changamoto zinazoikabili sekta ya elimu, Serikali ya ACT itaunda Tume ya Kitaifa ye Elimu yenye wajumbe wabobezi katika masuala ya elimu kutoka ndani na nje ya nchi ili kutathmini mfumo mzima wa elimu na kutoa mapendekezo ya mfumo bora zaidi utakaowawezesha watanzania kukabiliana na changamoto za Karne ya 21.



Copyright Freddy Feruzi

# 6. MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Ili serikali iweze kuwajibika kikamilifu katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa juu, itahitaji iwe na vyanzo vya uhakika vya mapato. Chanzo kikubwa cha mapato ya serikali ni kodi. Hivi sasa Serikali inakusanya mapato kwa kiwango kidogo sana kulinganisha na Pato la Taifa (GDP). Kwa mujibu wa takwimu mpya za uchumi zilizotolewa mapema mwaka huu, hivi sasa mapato ya kikodi ni 11% tu ya Pato la Taifa (GDP). Tafiti zinaonyesha kwamba ili serikali iweze kupata raslimali fedha za kuendesha Serikali ni lazima uwiano wa mapato ya kikodi kwa Pato la Taifa ifikie 25%. Hilo ndio lengo la Serikali itakayoongozwa na ACT. Ili kufikia lengo hili na kupata raslimali fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika ilani hii, Serikali ya ACT itachukua hatua zifuatazo:

**6.1 Kujenga uchumi wa kilimo na ufugaji** ukilenga kuwawezesha wakulima wadogo kuweza kugeuza kilimo kuwa mtaji wa biashara ili kilimo kiwe chanzo cha chakula na mahitaji muhimu ya kiuchumi na kijamii. Tanzania ni lazima ijenge uchumi wa kilimo cha wakulima wadogo wadogo chenye tija. Ili kufikia lengo hili, Serikali ya ACT itachukua hatua zifuatazo:

- Kuwapa wananchi mamlaka zaidi ya kisheria katika kumiliki ardhi katika ngazi ya kijiji
- Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ufugaji bora na wa kisasa ili kuleta tija



- Kutengeneza mipaka ya kisheria kuhusu umiliki wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji
- Serikali kufufua utaratibu wa kununua mazao ya chakula ya wananchi kwa ajili ya kuhifadhi
- Serikali itatenga maeneo maalum katika maeneo ya kikanda kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wa ACT serikali itatenga na kuyaendeleza mabonde matano katika kanda za Pwani, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa angalau asilimia 10 ya ardhi inatumika kwa kilimo cha umwagiliaji.
- Kuanzisha Bima ya Taifa ya Mifugo itakayowasaidia wafugaji kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa kitaalam
- Kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi na sekondari inakuwa na shamba la mfano
- Kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya teknolojia katika kilimo
- Kutenga bajeti maalum kwa ajili ya utafiti wa kilimo
- Kuongeza bajeti ya kilimo kama ilivyopendekezwa na Tamko la Maputo kuhusu umuhimu wa kuwa na akiba ya chakula cha ziada
- Mashamba yote yaliyobinafsishwa yatarejeshwa kwa wananchi kwa kuwagawia kwa mfumo wa 'outgrowers' scheme'. Itakuwa marufuku wawekezaji kuwakodishia wananchi ardhi bali wananchi watamilikishwa ardhi kwa utaratibu wa kisheria.
- Kuelekeza nguvu vijijini katika ujenzi wa miundo mbinu ya barabara na reli ili kuwezesha usafirishaji wa mazao na bidhaa zingine kutoka vijijini kuelekea kwenye masoko


**6.2 Kukuza utalii nchini ambayo ina nafasi kubwa ya kuchangia ukuaji wa uchumi na kuongeza fedha za kigeni** kwa kuchukua hatua zifuatazo:

- Kuitangaza Tanzania kama kituo cha utalii katika ukanda wa Afrika kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii angalau kufikia milioni tatu kwa mwaka
- Kutoa motisha wa kikodi ili kuhamasisha uwekezaji katika ujenzi wa mahoteli ili kupanua idadi ya vitanda katika mahoteli ili kukidhi mahitaji ya watalii
- Kuwekeza katika ujenzi wa miundo mbinu inayoelekea katika maeneo ya watalii
- Kutangaza maeneo mengine ya utalii na kuhamasisha watalii kuyatembelea hasa utalii katika ukanda wa nyanda za juu kusini
- Kuipa uwezo zaidi wa kifedha Bodi ya Taifa ya utalii ili kuweza kuendeleza utalii nyumbulishi

• Kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ya utalii ili kuvutia watalii, ikiwemo utunzanji wa mazingira katika maeneo ya utalii

• Kuendeleza njia mbadala za mapato kwa wakazi wanaoishi karibu na maeneo ya utalii ili wajione sehemu muhimu ya maeneo haya na kuwahamasisha wawe rafiki kwa mazingira ya utalii

• Kupiga vita uwindaji wa tembo na kuhamasisha kukomeshwa kwa biashara ya pembe za ndovu duniani



Copyright Freddy Feruzi



**6.3 Kuimarisha uongozi bora, kupiga vita rushwa na kusafisha uozo ili kudhibiti mapato na matumizi ya serikali** kwa kuchukua hatua zifuatazo:

• Kutekeleza kikamilifu sera ya serikali ya uwazi (Open Government Policy)

• Kuweka mazingira ya kisheria ili kuimarisha na kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari ili viweze kutoa habari za kweli na kwa wakati kwa wananchi kuhusu utendaji wa serikali

• Kuipa mamlaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mamlaka zaidi ya kukamata na kushtaki watu na taasisi wanaotuhumiwa kwa rushwa

• Kubadili mfumo wa kisheria kwenye masuala ya rushwa kwa kugeuza uthibitisho wa mali halali kutoka kwa Jamhuri kwenda kwa mtuhumiwa (reverse of burden of proof).

• Kuliunda upya Jeshi la Polisi ili kuliimarisha kitaalamu na kiweledi na kulinasua na umateka wa kisiasa ambao limo katika utawala wa sasa

• Kupiga marufuku mtu yeyote aliyepatikana na hatia ya kula rushwa kufanya kazi na/au biashara katika taasisi ya serikali

• Kuweka utaratibu wa kisheria utakaohakikisha kwamba makampuni yote yatakayopatikana na hatia ya kutoa na kupokea rushwa mali zao zinataifishwa

• Kuhuisha mchakato wa mabadiliko ya Katiba kuanzia pale iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilipoishia

• Kuibadili Taasisi ya Taaluma ya Mwalimu Nyerere (Kigamboni) kuwa Chuo cha Mafunzo ya Uongozi. Utawekwa utaratibu wa kisheria kuhakikisha kwamba sifa mojawapo ya mtu yeyote anayewania uongozi wa kitaifa \ kuanzia ubunge awe amepata mafunzo kutoka katika chuo hiki

• Kupanua wigo wa kodi kwa kuhakikisha kila raia mwenye kipato analipa kodi kwa kujaza ' tax returns' kila mwaka na kuweka mfumo Mpya wa kodi za kimataifa kuzuia makampuni ya kimataifa ( MNCs) kumomonyoa wigo wa kodi ( Base erosion and profit shifting ). Vile vile maduhuli yote ya Serikali yatakusanywa Kielektroniki na Hati zote za ardhi zitaunganishwa na namba ya mlipa kodi

• Kupitia upya mikataba ya uwekezaji katika maeneo ya raslimali ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano mzuri wa kimapato kati ya serikali na wawekezaji

• Kuipa uhuru na mamlaka zaidi ya kisheria Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuondoa uingiliwaji na viongozi wa kisiasa ili iweze kukusanya kodi kwa ufanisi zaidi.

- Kuandika upya sheria ya maadili ya Viongozi kwa kurejesha Miiko ya Uongozi na uwazi kwa umma wa Tamko la Maslahi, Mali na Madeni ya Viongozi
- Kujenga Mfumo Mpya wa uchumi usio wa kinyonyaji kwa kubomoa kabisa vikundi maslahi katika biashara (cartels) na hasa kwenye bidhaa kama nguo, Korosho, Sukari na Mchele.
- Mikataba yote inayohusu rasilimali za nchi kuwekwa wazi na lazima ipitishwe na kuidhinishwa na Bunge



# WIMBO WA TAIFA – (TANZANIA NATIONAL ANTHEM)




**Mungu Ibariki Afrika,**
**Wabariki Viongozi Wake,**
**Hekima, Umoja na Amani,**
**Hizi ni Ngao Zetu**
**Afrika na Watu Wake.**
**Ibariki, Afrika, Ibariki, Afrika,**
**Tubariki, Watoto wa Afrika**

**Mungu Ibariki Tanzania,**
**Dumisha Uhuru na Umoja,**
**Wake kwa Waume na Watoto,**
**Mungu, Ibariki, Tanzania na Watu Wake**
**Ibariki, Tanzania, Ibariki, Tanzania,**
**Tubariki, Watoto wa Tanzania.**